



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI



Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Jengo la Ukaguzi, 16 Barabara ya Samora Machel, S.L.P. 9080,
11101 Dar es Salaam. Simu ya Upepo: 'Ukaguzi' D'Salaam, Simu: 255(022)2115157/8,
Nukushi: 255(022)2117527, Barua pepe: ocag@nao.go.tz, Tovuti: www.nao.go.tz

TAARIFA KWA UMMA

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) Prof. Mussa Juma Assad jana tarehe 28 Machi, 2019 amemkabidhi Mheshimiwa Raisi wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli ripoti ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 June 2018.

Ripoti hiyo imewasilishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu katika hafla fupi iliyofanyika Ikulu Jijini Dar Es Salaam na kuhudhuriwa na Viongozi mbalimbali kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

Akizungumza baada ya kupokea ripoti hiyo, Mh. Rais John Magufuli ameipongeza ofisi ya CAG kwa kazi nzuri inayofanya na pia ameahidi kuwa Serikali itaendelea kushirikiana kwa karibu na Ofisi hiyo katika kukabiliana na kudhibiti matumizi mabaya na upotevu wa fedha za Umma.

Kwa Mujibu wa Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 143 kifungu kidogo 2 na 4 kinamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kukabidhi Ripoti hizo kwa Mheshimiwa Rais kabla ya Tarehe 31 Machi kila mwaka na baada ya hapo ripoti hiyo inawasilishwa bungeni siku saba za mwanzo za kikao cha Bunge kinachofuata.

Miongoni mwa ripoti zilizokabidhiwa kwa Mheshimiwa Rais ni Ripoti ya Ukaguzi wa Serikali kuu, Ripoti ya Ukaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, Ripoti ya Ukaguzi wa Mashirika ya Umma, Ripoti ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, Ripoti ya Ukaguzi wa

Mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi na Ripoti 11 za Ukaguzi wa Ufanisi katika Sekta mbalimbali ambazo ni;

- i. Usimamizi wa Shughuli za Ujenzi wa Miradi ya Umwagiliaji
- ii. Usimamizi wa Miradi ya Maji Vijijini,
- iii. Usimamizi wa Miradi ya Maji itokanayo na Visima Virefu
- iv. Matengenezo ya Mitambo ya Kuzalisha Umeme,
- v. Usimamizi wa Elimu kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum,
- vi. Usimamizi wa Mfumo wa Ununuzi wa Magari ya Serikali kwa pamoja,
- vii. Ufuatiliaji wa Shughuli za Ujenzi wa Majengo ya Mijini,
- viii. Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Afya za Rufaa na Dharura kwa Hospitali za Rufaa ngazi ya juu,
- ix. Upatikanaji na Usambazaji wa Pembejeo za Kilimo,
- x. Usimamizi wa Utoaji wa Huduma ya Bima ya Afya nchini na
- xi. Ufuatiliaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi wa Ufanisi.

IMETOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO